

# القرآن الحكيم

## QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by  
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy  
(Former Chief Kadhi of  
Zanzibar & Kenya)



Ina Aya 112

SURATUL ANBIYAA

Ina Makuru 7

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Imewakaribia watu hisabu yao (ya Kiama), nao wamo katika mghafala; wanakengeuka tu, (wanapuza).

اقْتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ

2. Hayawajii mawaidha mapya kutoka kwa Mola wao ila huyasikia, na hali wanafanya mchezo

مُعْرِضُونَ ۝

مَا يَا نَبِيَّهُمْ مِنْ ذِكْرٍ مِّن رَّبِّهِمْ وَمَا سَمِعُوا

3. Zimeghafilika nyoyo zao. Na wanasemezana kwa siri wale waliodhulumu (nafsi zao, wanaambizana hivi): "Ni nani huyu (Muhammad) isipokuwa ni binadamu tu kama nyinyi? Je, mnafika katika uchawi, (mnakiendea kiini macho) na hali nyinyi mnaona?"

وَهُمْ يَلْعَبُونَ ۝

لَاهِبَةً فُلُوقُهُمْ وَأَسْرَأَ النَّجْوَىٰ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ۗ

هَلْ هَذَا إِلَّا بَشْرٌ مِّثْلُكُمْ أَفَتَأْتُونَ السَّحَرَاءَ إِنَّمَا

تُبْصِرُونَ ۝

4. Alisema (Nabii Muhammad) "Mola wangu anayajua yanayosemwa mbinguni na ardhini; Naye ndiye Asikiaye, Ajuaye."

قَالَ رَبِّي يَعْلَمُ الْقَوْلَ فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ وَهُوَ

السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ۝

5. Lakini (makafiri) walisema: "(Hayo anayoyasimulia) ni ndoto zilizovurugika, (zilizokorogeka)." (Na pengine wanasema); "Bali ameyabuni (mwenyewe)". (Na mara nyengine tena husema): "Bali huyu ni mtunga mashairi tu (Na haya ndiyo mashairi yake). Basi atulettee Muujiza kama walivyotumwa (Mitume) wa kwanza."

بَلْ قَالُوا أَصْغَاتُ أَحْلَامٍ بَلِ اقْتَرَبَهُ بَلْ هُوَ

شَاعِرٌ ۖ فَلْيَأْتِنَا بِالْبَيِّنَاتِ كَمَا أُتِيَ الْأَوَّلُونَ ۝

6. Hawakuamini kabla yao (hawa Maqureshi) watu wa mji (wo wote ule) tuliouangamiza: Basi wataamini hawa? (Hawataamini).

مَا أَمَدَتْ قَبْلَهُمْ مِّن قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا أَفَهُمْ

يُؤْمِنُونَ ۝

7. Hatukuwatuma, (hatukuwapa Utume) kabla yako ila wanaume (wa kibinadamu, si Malaika); tuliowafunulia, (tuliowaletea Wahyi). Basi waulizeni wenye kumbukumbu (ya mambo ya zamani) ikiwa nyinyi hamjui.

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ إِلَّا رِجَالًا نُّوْحِي إِلَيْهِمْ

فَسَلِّطْنَا أَهْلَ الذِّكْرِ إِن كُنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ۝

8. Wala hatukuwajaalia (hao Mitume kuwa)

وَمَا جَعَلْنَاهُمْ جَسَدًا لَا يَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَمَا

1. Sura hii imepewa jina *Al Anbiyaa* kwa kuwa imeeleza habari za Manabii wengi.  
 3-5. Aya hizi zinaonyesha jinsi wasioamini walivyokuwa wakibabaika katika kutafuta ya kuutukania Uislamu.  
 8. Makafiri wa Kiqureshi wakijiitua pambani wakisema: "Kuna Mtume anayekula?" Ndiyo wanajibiwa hivi.

miili isiyokula chakula, wala hawakuwa wenye kukaa milele (wasife).

9. Kisha tukawasadikishia ahadi (ya kunusuriwa juu ya maadui zao). Na tukawaokoa wao na wale tuliowataka. (Nao ni wale waliowafuata). Na tukawaangamiza waliopita mpaka (waliowekewa).

10. Bila shaka tumekuteremshieni Kitabu ambacho muna ndani yake mauidha kwenu. Je! Hamfahamu?

11. Na mingapi tuliiharibu katika miji iliyokuwa ikidhulumu, (yaani watu wake walikuwa madhalimu). Na tukawaumba baadaye watu wengine.

12. Basi walipohisi tu adhabu yetu, mara walianza kuikimbia.

13. Msikimbie, na rudini katika yale mliyojistareheshea na (katika) maskani yenu; ili mkaulizwe.

14. Wakasema: "Ole wetu! (Eee adhabu yetu). Hakika tulikuwa madhalimu (wa nafsi zetu)!"

15. Na kukaendelea kulia kwao huku hata tukawafanya kama waliofyekwa, wakazimika pumzi, (wakafa).

16. Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyo baina yake kwa mchezo.

17. Kama tungalitaka kufanya mchezo, tungejifanyia sisi wenyewe, (tusingekutieni kati), kama tungekuwa wafanyao mchezo.

18. Bali (tulifanyalo ni hili:-) tunaitupa haki juu ya batili ikalivunja bufuru (fuvu) la kichwa chake; na mara (batili) ikatoweka, (ikaondoka); Na adhabu inakungojeeni kwa ajili ya haya mnyonena (kumsingizia Mwenyezi Mungu).

19. Na ni vyake (tu Mwenyezi Mungu) vilivyomo mbinguni na ardhini. Na walioko kwake, (Malaika) hawatakabari na kumuabudu wala hawachoki, (hawapumziki).

20. Wanamtukuza usiku na mchana, hawanyong'onyei (hawafanyi uvivu).

كَانُوا خُلْدِيَيْنَ ①

ثُمَّ صَدَقْتَهُمُ الْوَعْدَ فَأَجْنَبْنَهُمْ وَمَنْ نَشَاءُ  
وَ أَهْلَكْنَا السُّرْفِيْنَ ②

لَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ كِتَابًا فِيهِ ذِكْرُكُمْ أَفَلَا  
تَعْقِلُونَ ③

وَكَمْ قَصَمْنَا مِنْ قَرْيَةٍ كَانَتْ ظَالِمَةً  
وَ أَنْشَأْنَا بَعْدَهَا قَوْمًا آخَرِينَ ④

فَلَمَّا أَحْسَبُوا أَنَّ بَأْسَنَا إِذَا هُمْ مِنْهَا يَرْكُضُونَ ⑤

لَا تَرْكُضُوا وَارْجِعُوا إِلَى مَا أُتِرْتُمْ فِيهِ وَمَسْكِنِكُمْ  
لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ⑥

قَالُوا يَا وَيْلَنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ⑦

فَمَا زَالَتْ تِلْكَ دَعْوَاهُمْ حَتَّى جَعَلْنَاهُمْ  
حَصِيدًا خَمِيدِينَ ⑧

وَ مَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَ الْأَرْضَ وَ مَا بَيْنَهُمَا لِعِبَادٍ ⑨

لَوْ أَرَدْنَا أَنْ نَتَّخِذَ لَهُمْ لَهْوًا لَوَلَّاهُ مَا نَحَدْنَا مِنْ  
لُدُنَّا ؕ إِن كُنَّا فَعِلِينَ ⑩

بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ فَيَدْمَغُهُ فَإِذَا  
هُوَ رَاقٍ ، وَ لَكُمْ الْوَيْلُ مِمَّا تَصِفُونَ ⑪

وَلَهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَ الْأَرْضِ ، وَ مَنْ عِنْدَهُ لَا  
يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِهِ ، وَ لَا يَسْتَحْسِرُونَ ⑫

يَسْبَحُونَ اللَّيْلَ وَ النَّهَارَ لَا يَفْتُرُونَ ⑬

Katika hii Aya walioifanya ya 9 wanatia vile vile upinzani wa kukaa Nabii Isa mbinguni, Kisha kuteremka. Sisi tumekwisha kubainisha mara nyingi kuwa hivi ndivyo alivyotwambia Mtume, kama ilivyosihhi kwa Hadithi za Al Bukhary na nyinginezo. Basi sisi juu yetu ni kufuata alivyotwambia Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

21. Au wamepata waungu katika ardhi wafufuao, (kwa hivyo wamewafanya ndio waola wao badala ya Mwenyezi Mungu)?

22. Lau kama wangalikuwako humo (mbinguni na ardhini) waungu (wengine) isipokuwa Mwenyezi Mungu: bila shaka zingeharibika (hizo mbingu na ardhi). Na ametakasika Mwenyezi Mungu, Mola wa Arshi, (yu mbali) na yale wanayomsifu kwayo.

23. Haulizwi (Mwenyezi Mungu) anayoyafanya (kwani yote ni ya haki) lakini wao (viumbe) wataulizwa.

24. Au wameshika badala yake miungu (iliyo kama Mwenyezi Mungu)? Sema: "Leteni dalili zenu." Haya (ninayokwambieni) ni ukumbusho wa hawa walio pamoja nami, na ukumbusho wa wale wa kabla yangu. Lakini wengi wao hawajui ya kweli, kwa hivyo wanapuzza.

25. Na hatukumtuma kabla yako Mtume yoyote ila tulimfunulia ya kwamba hakuna aabudiwaye ila Mimi, basi Niabuduni.

26. Na makafiri wanasema: "(Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema amejifanyia mtoto." Ametakasika (Mwenyezi Mungu!) Bali (hao Malaika) ni waja (wa Mwenyezi Mungu) waliotukuzwa

27. Hawamtangulii kwa neno (lake analosema), Nao wanafanya amri zake (zote).

28. (Mwenyezi Mungu) anayajua yaliyo mbele yao (hao Malaika) na yaliyo nyuma yao. Na (Hao Malaika) hawamuombi (yoyote) ila yule anayemridhia (Mwenyewe Mwenyezi Mungu), nao kwa ajili ya kumuogopa wananyenyekea.

أَمْ اتَّخَذُوا آلِهَةً مِّنَ الْأَرْضِ هُمْ يُنشِرُونَ ﴿٢١﴾

كَلَّا إِنَّ فِيهَا آلِهَةً إِلَّا اللَّهُ كَفَسَدَتَا،  
فَسُبْحَانَ اللَّهِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿٢٢﴾

لَا يُسْئَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْئَلُونَ ﴿٢٣﴾

أَمْ اتَّخَذُوا مِن دُونِ آلِهَةٍ قُلًا هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ،  
هَذَا إِذْ كُفِّرْتُمْ، بَلَىٰ أَكْثَرُهُمْ  
لَا يَعْلَمُونَ ۗ الْحَقُّ لَهُمْ مُعْرَضُونَ ﴿٢٤﴾

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ  
أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢٥﴾  
وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا سُبْحَانَهُ، بَلْ عِبَادٌ  
مُّكْرَمُونَ ﴿٢٦﴾

لَا يَسْئَلُونَكَ بِالْقَوْلِ وَهُمْ بِأَمْرِهِ يَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا  
يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنِ ارْتَضَىٰ وَهُم مِّنْ خَشْيَتِهِ  
مُسْتَفْقُونَ ﴿٢٨﴾

22. Hii ni kawaida isiyoanguka kuwa "Mafahali Wawili Hawakai Zizi Moja." Basi wangekuwako waungu wawili wangepigana daima hata mmoja amshinde mwenziwe au wauwane; udhia wishe. Na muda wote huo — wa kuzatiti vita mpaka kutiana mikononi — hawatashughulikia jingine ila hilo tu la kutafuta kushinda. Tena mambo atayaendesha nani?

Na wakiwa wengi zaidi kuliko wawili ndiyo vivyo — watapigana mpaka wamalizane. Au — tuseme U wapatane. Na wakipatana basi watauparaganya tu mwenesho wa ufalme wao kwani kwa "Manahodha Wengi Jahazi huzama."

Basi Mwenyezi Mungu ni Mmoja tu *Wahdahuu Laa Sharyka Lahuu.*

Na watu mambo yao ndiyo vivi hivi. Yakiwa yanaendesha na chungu ya wakubwa — na kila mmoja hakubali kumsikiliza mwenziwe — basi yataharibika tu. Ndiyo maana Mtume akihimiza kuwa sharti — katika kila mkusanyiko — apatikane mkubwa anayetiwa na wote kwa anayoyasema yakaingia Shariani; au akilini yakiwa hayahusu Sharia. Akisema Mtume kuwa watu — wakishakuwa watatu — katika msafara wao — basi sharti wamfanye mmoja mkubwa wao kwani mambo hayatengenci yakiwa fujo, ovyo ovyo, hayana mkubwa. Inasemwa kwa Kiarabu: *Laa yasluhunaasu Fawdhaa Laa saraatalqhum* yaani Mambo hayatengenci yakiwa ovyo, hayana mkubwa au wakubwa, wa kuyaendesha.

Na sharti ya hao wakubwa — ilivyoweka Uislamu — ni wawe na ilimu nzuri na utambuzi kamili. Ikiwa si hivyo, si wakubwa hao, wala mambo hayataendelea. Inasemwa: *Wala saraata Idhaa Fuhhaaluhum saaduu.*

23. Mwenyezi Mungu haulizwi, kwani yote anayofanya kuwafanyia waja wake, anawafanyia kwa INSAFU.

29. Na atakayesema miongoni mwao: "Mimi ni mungu, badala yake," basi huyo tutamlipa (kwa kumtia katika) Jahanamu. Hivi ndivyo tuwalipavyo madhalimu.

30. Je! hawakuona wale waliokufuru ya kwamba mbingu na ardhi vilikuwa vimeambatana, kisha tukaviambua, (tukavipambanua): Na tukafanya kwa maji kila kitu kilicho hai. Basi jee hawaamini?

31. Na tukaweka katika ardhi milima (yenye kuthubuti barabara katika ardhi) ili isiwayumbishe, na tukaweka humo mabarabara, wazi-wazi ili wapate kuongoza njia.

32. Na tukaifanya mbingu kuwa dari iliyohifadhiwa, lakini wanazikengeuka ishara Zake (Mwenyezi Mungu).

33. Na yeye ndiye aliyeumba usiku na mchana na jua na mwezi; vyote vinaogelea katika duara (zao).

34. Nasi hatukumfanya mwanadamu yoyote wa kabla yako aishi milele. Basi kama ukifa wewe wao wataishi milele?

35. Kila nafsi itaonja mauti, na tunakufanyieni mitihani kwa (mambo ya) shari na ya kheri; na kwetu (nyote) mtarejeshwa.

36. Na wanapokuona wale waliokufuru hawakufanyi chochote ila (kiombe cha kucheza) shere, (wakisema): 'Je! Huyu ndiye anayewataja waungu wenu (kwa vibaya)?' Na hao ndio wanaomkanusha Mwenyezi Mungu Mwenye Rehema.

37. Mwanadamu ameumbwa kwa (kupenda mambo yake yote yatokee kwa) haraka. Karibuni hivi nitakuonyesheni Ishara zangu, kwa hivyo msinihimize (kukuleteeni adhabu).

30. Mambo mawili haya (a) Kuwa mbingu na nchi zilikuwa kitu kimoja zikapambanuliwa, na (b) Kuwa kila kilicho hai kimefanywa kwa maji, ambayo hawakuyajuwa wenye ilimu za kisasa ila jana na juzi, yametangulia kutajwa katika Qurani tokea karne 14 zilizopita. Sasa wanasema kuwa Asilimia 66 (66%) za kiwiliwili cha Binadamu ni maji.

Na kadhalika yatakayotajwa katika Aya 33 ya sura hii. Na vile vile habari za broadcasting na television na yaliyo kama haya; yametajwa katika Qurani tangu Aya ya 44 ya *Suratul Aaraf* mpaka ya 50. Na kama habari za kukhitalifu daima kutoka na kuchwa jua katika ulimwengu mzima. Yametajwa haya katika Aya ya 40 ya *Suratul Maarij*. Na kuwa kuna jike na dume katika kila kitu: vyenye uhai na visivyo na uhai, kama ilivyo katika Aya ya 36 ya *Surat Yasin*. Na kama haya ya kuthubutisha kuwa kila kilichosemwa ndani ya Qurani ni kweli tu, isiyoweza kupingika, kama ilivyo katika Aya ya 53 ya *Surat Haa Mym Sajdah*.

33. Haya yanathubutisha haya ambayo ndiyo kwanza yanasemwa sasa.

وَمَنْ يَقْبَلْ مِنْهُمْ إِلَىٰ إِلَهِ مِنْ دُونِهِ فَذَلِكَ نَجْزِيهِ جَهَنَّمَ كَذَلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٣٠﴾

أَوَلَمْ يَرِ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ كَانَتَا رَتْقًا فَفَتَقْنَاهُمَا وَجَعَلْنَا مِنَ الْمَاءِ كُلَّ شَيْءٍ حَيًّا أَفَلَا يُؤْمِنُونَ ﴿٣١﴾

وَجَعَلْنَا فِي الْأَرْضِ رَوَاسِيًا أَنْ تَمِيدَ بِهِمْ وَجَعَلْنَا فِيهَا فِجَاجًا سُبُلًا لَعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ ﴿٣٢﴾

وَجَعَلْنَا السَّمَاءَ سَقْفًا مَحْفُوظًا وَهُمْ عَنْ آيَاتِهَا مُعْرِضُونَ ﴿٣٣﴾

وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٣٤﴾

وَمَا جَعَلْنَا لِבَشَرٍ مِنْ قَبْلِكَ الْخُلْدَ أَفَأَنْ تَمُنَّ بِقَهُمُ الْخُلْدُونَ ﴿٣٥﴾

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ وَنَبْلُوكُمْ بِالشَّرِّ وَالْخَيْرِ فِتْنَةً وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ﴿٣٦﴾

وَإِذَا رَأَى الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ يَنْجِدُونَكَ إِلَّا هُزُوعًا ۗ أَلْهَذَا الَّذِي يُدَّكِرُ الْهَيْكَلَكُمْ ۗ وَهُمْ بِذِكْرِ الرَّحْمَنِ هُمْ كَافِرُونَ ﴿٣٧﴾

خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَاقٍ ۗ سَآوِرٍ يَكُمُرُ آيَاتِي فَلَا تَسْتَعْجِلُونِ ﴿٣٨﴾

38. Na wanasema (makafiri): "Ahadi hii (yakuadhibiwa) itatokea lini kama mnasema kweli?"

وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٨﴾

39. Lau wangejua wale waliokufuru (adhabu itakayowapata) wakati ambao hawatazuia Moto katika nyuso zao wala katika migongo yao wala hawatasaidiwa, (wasingesema haya).

لَوْ يَعْلَمُ الَّذِينَ كَفَرُوا حِينَ لَا يَكْفُونَ عَنْ وُجُوهِهِمُ النَّارَ وَلَا عَنْ ظُهُورِهِمْ وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٣٩﴾

40. Bali utawafikia kwa ghafla na utawaduwalisha (danganisha), kisha hawataweza kuurudisha, wala hawatapewa muhula.

بَلْ تَأْتِيهِمْ بَغْتَةً فَتَبْهَتُهُمْ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ رَدَّهَا وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٤٠﴾

41. Na bila shaka walichezwa shere, (walifanyiwa dhihaka) Mitume waliokuwa kabla yako; kwa hivyo wale waliofanya dhihaka miongoni mwao yaliwafika yale waliyokuwa wakiyafanya dhihaka.

وَلَقَدْ اسْتَهْزَيْتُمْ بِرُسُلِ مِن قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِينَ سَخِرُوا مِنْهُمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٤١﴾

42. Sema: "Nani anayeweza kukulindeni usiku na mchana na (adhabu ya) Mwenyezi Mungu?" Bali wao wanapuzza kumkumbuka Mola wao.

قُلْ مَنْ يَكْلُمُ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ مِنَ الرِّجْمِ، بَلْ هُمْ عَنْ ذِكْرِ رَبِّهِمْ مُعْرِضُونَ ﴿٤٢﴾

43. Je, wanao miungu wanaowalinda badala yetu? Hawawezi kujisaidia wenyewe (waungu hao; wataweza kusaidia watu wengine)? Wala (waungu hao) hawatahifadhiwa nasi (tukitaka kuwatesa).

أَمْ لَهُمُ إِلَهَةٌ تَمْنَعُهُمْ مِن دُونِنَا لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَ أَنفُسِهِمْ وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٤٣﴾

44. Bali tuliwastarehesha (makafiri) hawa na baba zao mpaka umri wao umetawilika, (umekuwa mrefu) juu ya hayo. Je, hawaoni ya kwamba tunaiendea ardhi yao tukiipunguza mipaka yake? Basi je! wao ni wenye kushinda?

بَلْ مَتَمَنَّا أَهْلَؤَلَاءِ وَأَبَاءَهُمْ حَتَّىٰ طَالَ عَلَيْهِمُ الْعُمُرُ، أَفَلَا يَرَوْنَ أَنَّ نَارَ الْأَرْضِ تَنقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا، أَفَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿٤٤﴾

45. Sema: "Mimi nakuonyeni kwa (maneno ya) Wahyi (wa Mwenyezi Mungu)" Na viziwi hawasikii mwito wanapoonywa.

قُلْ إِنَّمَا أُنذِرُكُمْ بِالْوَحْيِ وَلَا يَسْمَعُ الصَّمُّ الدُّعَاءَ إِذَا مَا يُنذَرُونَ ﴿٤٥﴾

46. Na kama ingaliwagusa dharuba moja tu ya adhabu ya Mola wako, bila shaka (wangalinyenyekka mara moja) wakasema: "Eee adhabu yetu! Hakika tulikuwa madhalimu!"

وَلَكِنَّ مَسَّهُمُ نَفْسٌ مِّنْ عَذَابِ رَبِّكَ لَيَقُولُنَّ يَٰوَيْلَنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٤٦﴾

47. Nasi tutaweka mizani za uadilifu siku ya Kياما, na nafsi yoyote haitadhulumiwa hata kidogo. Na hata kama likiwa (jambo hilo lina) uzito mdogo wa chembe ya hardali nalo tutalileta; Nasi tunatosha kuwa wajuzi (wazuri kabisa) wa hisabu.

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا، وَإِنْ كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا، وَكُنَّا بِهَا حَسِيبِينَ ﴿٤٧﴾

48. Na kwa yakini tuliwapa Musa na Haruni (kitabu kilicho) kipambanuzi na muanga na mauidha kwa wacha-Mungu

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ وَهَارُونَ الْفُرْقَانَ وَضِيَاءً وَذِكْرًا لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٤٨﴾

47. Hardali (Haridali) ni punje tembe (shembe) ndogo kuliko ya mawele.

49. Ambao wanamuogopa Mola wao (hata) wanapokuwa faraghani, na pia hukio gopa Kiama.

50. Na hii (Qurani) ni mauidha yaliyo barikiwa, tuliyoyateremsha (kwako). Basi: Je! nyinyi mnayakanusha?

51. Na hakika tulimpa Ibrahimu uwongofu wake zamani na tulikuwa tukimjua (vizuri).

52. (Wakumbushe watu) alipomwambia baba yake na watu wake: "Ni nini masanamu haya mnayakalia wakati wote (kuya-abudu)?"

53. Wakasema, "Tuliwakuta babu zetu wakiyaabudu, (basi na sisi tunayaabudu)."

54. Akasema: "Bila shaka nyinyi na baba zenu mulikuwa katika upotofu (upotevu) ulio dhahiri."

55. Wakasema: "Je! Umetujia kwa (maneno ya) haki au umo miongoni mwa wachezaji?"

56. Akasema: "(Siyo! mimi si mchezaji) Bali Mola wenu ni yule Mola wa mbingu na ardhi ambaye ndiye aliyeziumba. Nami ni miongoni mwa wenye kuyashuhudia haya."

57. "Na Wallahi (Kwa haki ya Mungu) nitayafanyia mabaya masanamu yenu haya baada ya kunipa mgongo mkenda zenu."

58. Basi akayavunja (masanamu yote yale) vipande vipande isipokuwa lile kubwa lao (aliliacha), ili wao (hao makafiri) walirudie.

59. Wakasema: "Nani aliyeifanya hivi miungu yetu? Hakika huyo yu miongoni mwa madhalimu (wakubwa)?"

60. Wakasema: "Tulimsikia kijana mmoja akiwataja anayeitwa Ibrahimu."

61. Wakasema: "Basi mleteni mbele ya macho ya watu, wamshuhudie (kwa ubaya wake huo)."

62. Wakasema: "Je! Wewe umeifanya hivi miungu yetu, ee Ibrahimu?"

63. Akasema: "Siyo, Bali amefanya (hayo) huyu mkubwa wao, basi (muulizeni na) waulizeni (pia hao waliovunjwa) kama wanaweza kunena!"

63. Wametia uwongo wao katika maelezo ya Aya hii waliyoifanya kuwa ni ya 64 na wakasingizia kuwa Ar Raazy ametia nguvu kauli hiyo ambayo dhahiri ya Qurani hapo haisaidii hata chembe kama ilivyobainishwa katika sahifa ya 60 ya Juzuu ya 17 ya *Ruhul Maany*. Wanadanganya kusudi.

الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ وَهُمْ مِنَ السَّاعَةِ مُشْفِقُونَ ﴿٥٩﴾

وَهَذَا ذِكْرُ مُوسَى إِذْ أُنزِلَتْ لَهُ آفَاتُنَا لَهُ مُكْرِمُونَ ﴿٦٠﴾

وَلَقَدْ آتَيْنَا إِبْرَاهِيمَ رُسُدَهُ مِنْ قَبْلُ وَكُنَّا بِهِ عَلِيمِينَ ﴿٦١﴾

إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَا هَذِهِ السَّمَائِيلُ الَّتِي أَنْتُمْ لَهَا عَاكِفُونَ ﴿٦٢﴾

قَالُوا وَجَدْنَا آبَاءَنَا لَهَا عَابِدِينَ ﴿٦٣﴾

قَالَ لَقَدْ كُنْتُمْ أَنْتُمْ وَآبَاؤُكُمْ فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٦٤﴾

قَالُوا أَجِئْتَنَا بِالْحَقِّ أَمْ أَنْتَ مِنَ اللَّاعِبِينَ ﴿٦٥﴾

قَالَ بَلْ رَبُّكُمْ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ الَّذِي فَطَرَهُنَّ وَأَنَا عَلَىٰ ذِكْمٍ مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٦٦﴾

وَ تَاللَّهِ لَأَكِيدَنَّ أَصْنَامَكُمْ بَعْدَ أَنْ تُوَلُّوا مُدْبِرِينَ ﴿٦٧﴾

فَجَعَلَهُمْ جُودًا إِلَّا كِبِيرًا لَهُمْ لَعَلَّهُمْ إِلَيْهِ يَرْجِعُونَ ﴿٦٨﴾

قَالُوا مَنْ فَعَلَ هَذَا بِالْهَيْتِنَا إِنَّهُ لَمِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٦٩﴾

قَالُوا سَمِعْنَا فَتًى يَذُكُرُهُمْ يُقَالُ لَهُ إِبْرَاهِيمُ ﴿٧٠﴾

قَالُوا فَأْتُوا بِهِ عَلَىٰ أَعْيُنِ النَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَشْهَدُونَ ﴿٧١﴾

قَالُوا أَنْتَ فَعَلْتَ هَذَا بِالْهَيْتِنَا يَا إِبْرَاهِيمُ ﴿٧٢﴾

قَالَ بَلْ فَعَلَهُ كَبِيرُهُمْ هَذَا فَسَاءَ لَهُمْ إِنْ كَانُوا يَنْظُرُونَ ﴿٧٣﴾

64. Basi wakajirudi nafsi zao, (wakafikiri udhalilifu wa waungu hao walio nao, wasioweza kujipigania) na wakasema: "Hakika nyinyi mlikuwa madhalimu (wa nafsi zenu kwenda kuwaabudu wasiokuwa na maana)."

65. Kisha wakainamishwa vichwa vyao, (wakarejea ujingani, ukafirini, wakasema): "Hakika umekwishajua ya kwamba hawasemi, (kwa nini unatucheza shere?)."

66. Akasema: "Je! Mnaabudu badala ya Mwenyezi Mungu (miungu) isiokufaeni chochote (mnapowaabudu) wala kukudhuruni (chochote mnapoacha kuwaabudu)?"

67. Kefule (udhalilifu) yenu na ya hivyo mnavyoviabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu. Je! hamfikiri?

68. Wakasema: "Mteketezeni kwa moto na mwinusuru miungu yenu, ikiwa nyinyi ni watendao jambo (basi tendeni hili)."

69. Tukasema: "Ewe moto! Kuwa baridi na salama juu ya Ibrahimu"

70. Na walimtakia ubaya, lakini tukawafanya wao ndio wenye kupata hasara.

71. Na tulimuokoa yeye na Luti (tukawapeleka katika ardhi tuliyoibarikia kwa ajili ya walimwengu. (Ardhi ya Shamu).

72. Naye (Ibrahimu) tukampa Is-haka (kuwa ni mtoto wake) na Yaakubu kuwa mjukuu; na wote tukawafanya kuwa wema.

73. Na tukawajaalia kuwa Maimamu wanaoongoza kwa amri yetu, na tukawapeleka Wahyi (tukawafunulia), wa kuzifanya kheri na kusimamisha Sala na kutoa Zaka. Na walikuwa kwetu ni wenye kutunyenyeka.

74. Na Luti tukampa hukumu na ilimu na tukamuokoa na (watu wa) ule mji uliokuwa ukifanya maovu. Bila shaka wao walikuwa watu wabaya, wavunjao amri

75. Na tukamuingiza (huyu Luti) katika rehema yetu. Hakika yeye alikuwa miongoni mwa wafanyao mema.

76. Na (wakumbushe) Nuhu alipotulingania zamani (kutuomba), nasi tukamuitikia, na

فَرَجَعُوا إِلَىٰ أَنفُسِهِمْ فَقَالُوا لَوْلَا إِلَهُكُمُ اللَّهُ  
الظالمون ﴿٣٦﴾

ثُمَّ نَكَّسُوا عَلَىٰ رُءُوسِهِمْ؛ لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا هَؤُلَاءِ  
بَيِّنَاتُونَ ﴿٣٧﴾

قَالَ أَفَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُكُمْ شَيْئًا  
وَلَا يَضُرُّكُمْ ﴿٣٨﴾

أَفِ لَكُمْ وَلِمَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ أَفَلَا  
تَعْقِلُونَ ﴿٣٩﴾

قَالُوا حَرِّقُوهُ وَانصُرُوا آلِهَتَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ  
فَاعِلِينَ ﴿٤٠﴾

قُلْنَا يَا نَارُ كُونِي بَرْدًا وَسَلَامًا عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ﴿٤١﴾

وَأَرَادُوا بِهِ كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْآخِزِينَ ﴿٤٢﴾

وَنَجَّيْنَاهُ وَلُوطًا إِلَى الْأَرْضِ الَّتِي بَارَكْنَا  
فِيهَا لِلْعَالَمِينَ ﴿٤٣﴾

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ نَافِلَةً  
وَكُلًّا جَعَلْنَا صَالِحِينَ ﴿٤٤﴾

وَجَعَلْنَاهُمْ آيَةً لِّیَهْدُونَ بِأَمْرِنَا وَأَوْحَيْنَا  
إِلَيْهِمْ فِعْلَ الْخَيْرَاتِ وَإِقَامَ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءَ  
الرِّزْقِ: وَكَانُوا لَنَا عِبِيدِينَ ﴿٤٥﴾

وَلُوطًا إِتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعَلَّمْنَاهُ نَجَاتَهُ مِمَّن  
الْقَرِيبَةِ الَّتِي كَانَتْ تَعْمَلُ الْخَبِيثَاتِ وَالَّذِينَ  
كَانُوا قَوْمًا سَوِيًّا فَيَقِينُ ﴿٤٦﴾

وَأَدْخَلْنَاهُ فِي رَحْمَتِنَا إِنَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٤٧﴾

وَنُوحًا إِذْ نَادَىٰ مِن قَبْلِ فَاسْتَجَبْنَا لَهُ فَنَجَّيْنَاهُ

tukamuokoa yeye na watu wake katika shida (msiba) kubwa hiyo.

77. Na tukamnusuru juu ya watu waliozikadhibisha Aya zetu. Hakika wao walikuwa watu wabaya. Basi tukawatotesha (gharikisha) wote.

78. Na (wakumbushe) Daudi na Suleimani walipokata hukumu juu ya konde, walipolisha humo mbuzi wa watu usiku. Nasi kwa hukumu yao hiyo tulikuwa Mashahidi, (tunaona tunasikia)

79. Tukamfahamisha Suleimani (kuliko mzee wake, Daudi). Na kila mmoja tulimpa hukumu na ilimu. Na tukatiisha milima (iwe) pamoja na Daudi, ikimtukuza Mwenyezi Mungu (Na tukamtiishia) ndege pia (wawe wakimtukuza Mwenyezi Mungu pamoja naye), Na sisi ni wafanyayo (tuyatakayo).

80. Na tukamfundisha (Daudi) matengenezo ya mavazi ya vita kwa ajili yenu ili yakuhifadhini katika mapigano yenu. Je! Mtakuwa wanaoshukuru?

81. Na kwa Suleimani (tukautiisha) upepo wa nguvu uendao kwa amri yake katika ardhi ambayo tumeibarikia, (Shamu). Nasi ndio tunaokijua kila kitu.

82. Na (tukamtiishia) mashetani wenye kumpigia mbizi (ili wamletee lulu) na wakimfanyia vitendo vyengine visivyokuwa hivyo. Nasi tulikuwa Walinzi wao.

83. Na (Mtaje) Ayyubu, alipomwita Mola wake (akasema) "Mimi imenipata dhara, nawe ndiwe Unayerehemu kuliko wote wanaorehemu."

84. Basi tukamkubalia (wito wake) na tukamuondolea dhara aliyokuwa nayo, na tukampa watu wake na mfano wao pamoja nao. Ni rehema inayotoka kwetu, na ukumbusho (mzuri) kwa wafanyao ibada.

85. Na (Mtaje) Ismaili, na Idrisi, na Dhul-Kifli —wote walikuwa miongoni mwa wanaosubiri.

86. Na tukawaingiza katika rehema yetu. Hakika wao walikuwa katika watu wema.

87. Na (Mtaje) Dhun-Nun (Yunusi) alipoondoka hali amechukiwa, na akadhani ya kwamba hatutamdhikisha. Basi (alipozongwa) aliita katika giza (akasema): "Hakuna aabudiwaye isipokuwa wewe, Mtakatifu; hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu (nafsi zao)."

وَأَهْلَهُ مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيمِ ۝

وَوَصَّيْنَاهُ مِنَ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا  
إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا سَوِيًّا فَآغْرَقْنَاهُمْ أَجْمَعِينَ ۝

وَدَاوُدَ وَ سُلَيْمَانَ إِذْ يَخْتَلِمُ فِي الْحَرَّةِ إِذْ  
لَفَّشَتْ فِيهِ جَمْعُ الْقَوْمِ وَكُنَّا لِحَكِيمِهِمْ  
شَاهِدِينَ ۝

فَفَهَّمْنَاهَا سُلَيْمَانَ وَكُلًّا آتَيْنَاهُمْ حُكْمًا وَعِلْمًا  
وَسَخَّرْنَا مَعَ دَاوُدَ الْجِبَالَ يُسَبِّحْنَ وَالطَّيْرَ وَكُنَّا  
فَاعِلِينَ ۝

وَعَلَّمْنَاهُ صَنْعَةَ لَبُوسٍ لَكُمْ لِنَحْصِنَكُم مِّنْ  
بَأْسِكُمْ فَهَلْ أَنْتُمْ شَاكِرُونَ ۝

وَلِسُلَيْمَانَ الرِّيحَ عَاصِفَةً تَجْرِي بِأَمْرِهِ إِلَى  
الْأَرْضِ الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا وَكُنَّا بِكُلِّ شَيْءٍ  
عَلِيمِينَ ۝

وَمِنَ الشَّيْطَانِ مَن يُغْوِصُونَ لَهُ وَيَعْمَلُونَ عَمَلًا  
ذُونَ ذَلِكَ وَكُنَّا لَهُمْ حَافِظِينَ ۝

وَ أَيُّوبَ إِذْ نَادَى رَبَّهُ أَنِّي مَسَّنِيَ الضُّرُّ وَ  
أَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ۝

فَأَسْتَجَبْنَا لَهُ فَكَشَفْنَا مَا بِهِ مِنْ ضُرِّهِ وَأَيُّوبَ  
أَهْلَهُ وَمِثْلَهُمْ مَعَهُمْ رَحْمَةً مِنَّا عَسَدْنَا  
وَذِكْرًا لِّلْعَبِيدِينَ ۝

وَإِسْمَاعِيلَ وَإِدْرِيسَ وَذَا الْكِفْلِ كُلٌّ مِّنَ  
الضَّالِّينَ ۝

وَإَدْخَلْنَاهُمْ فِي رَحْمَتِنَا إِنَّهُمْ مِّنَ الصَّالِحِينَ ۝

وَذَا النُّونِ إِذْ ذُهِبَ مُغَاصِبًا فَظَنَّ أَنْ لَنْ  
نَقْدِرَ عَلَيْهِ فَنَادَى فِي الظُّلُمَاتِ أَنْ لَا إِلَهَ  
إِلَّا أَنْتَ سُبِّحْنَاكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ۝

88. Basi tukampokelea na tukamuokoa katika huzuni ile. Na namna hivyo ndivyo tuwaokoavyo walioamini.

فَاسْتَجَبْنَا لَهُۥ وَوَجَّيْنَاهُ مِنَ الْعَمَمِ ۖ وَكَذَلِكَ نُنْجِي الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٨﴾

89. Na (Mtaje) Zakaria alipomwita Mola wake (akasema) “Mola wangu! Usiniache peke yangu na wewe ndiwe Mbora wa wanaorithi.”

وَرَكِبْنَا إِذْنًا دُۢمُۥ رَبِّهِۦ لَا تَدْرِي قَوْلًا ؕ وَأَنْتَ حَيَّرَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٨٩﴾

90. Basi tukampokelea (dua yake) na tukampa Yahya na tukamponyeshea, (tukampozea) mkewe. Bila shaka wao walikuwa wepesi wa kufanya wema, na wakituomba kwa shauku na khofu. Nao walikuwa wakitunyenyekoa.

فَاسْتَجَبْنَا لَهُۥ وَوَهَبْنَا لَهُۥ يَحْيَىٰ وَاصَدَقْنَا لَهُۥ زَوْجَهُۥ إِنَّهُمْ كَانُوا يُسْرِعُونَ فِي الْحَيْرَاتِ وَبَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا ۖ وَكَانُوا لَنَا خِشَعِينَ ﴿٩٠﴾

91. Na (Mtaje yule mwanamke) aliyejilinda, (aliyehifadhi) nafsi yake, na tukampulizia roho yetu na tukamfanya yeye na mwanawe kuwa miujiza (ya kudra ya Mwenyezi Mungu) kwa walimwengu.

وَالَّتِي أَحْصَدَتْ فَرْجَهَا فَتَنَحْنَا فِيهَا مِنْ رُوحِنَا وَجَعَلْنَاهَا وَابْنَهَا آيَةً لِلْعَالَمِينَ ﴿٩١﴾

92. (Tuliwaambia wote hao:) “Kwa yakini huu umma wenu ni umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu (mmoja), kwa hivyo Niabuduni.”

إِنَّ هَذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً ۖ وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُونِ ﴿٩٢﴾

93. Nao wakalivunja jambo lao hili baina yao, (wakafarikiana): Wote watarudia kwetu.

وَتَقَطَّعُوا أَمْرَهُمْ بَيْنَهُمْ كَلَّالِإِنَّا رَاجِعُونَ ﴿٩٣﴾

94. Na atakayefanya vitendo vizuri, hali ya kuwa Muislamu, basi haitakataliwa juhudi yake (hiyo); Na hakika Sisi tunamuandikia (yote hayo anayoyafanya).

فَمَنْ يَعْمَلْ مِنَ الصَّالِحَاتِ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَا كُفْرَانَ لِسَعِيهِ ۖ وَإِنَّا لَهُ كَاتِبُونَ ﴿٩٤﴾

87. Nabii Yunusi katika Qurani ameitwa kwa majina matatu: “Yunus,” “Dhun Nun,” na “Sahibul Hut.” Haya mawili ya mwisho ambayo maana yake ni “Mwenye kumezwa na samaki,” yanaashiria kisa kilichotajwa katika *Sura Assaffaat*.

90. Maneno haya ya Mwenyezi Mungu yanayosema katika kuwasifu hawa Mitume — kuwa walikuwa wakituabudu na kutuomba kwa ajili ya shauku ya (Pepo) na khofu ya (Moto)—yanapinga maneno yanayosifiwa katika vitabu vya Tasawwuf kuwa daraja kubwa ni kumuabudu Mwenyezi wivi hivi kwa kuwa anastahiki kuabudiwa tu, si kwa kutaraji Pepo wala kuogopa Moto. Na wakasema kuwa hivi ndivyo walivyokuwa wakiabudu Kina Mabwana Fulani. . . na Mabibi Fulani. Basi Mwenyezi Mungu sivyo alivyowasifu Mitume yake hivyo. Na Qurani yote nzima inatwambia kuwafuata hao aliowataja yeye—kama ilivyo katika Aya nyingi, kama Aya ya 90 ya *Suratul An-am*, na Aya ya 4 na ya 6 za *Suratul Mumtahina*.

Na kwa ajili ya kutaraji hivi na kuogopa hivi—kutaraji rehema ya Mwenyezi Mungu na kuogopa adhabu yake—ndivyo walivyofasiri wafasiri maulamaa, wa mwanzo kabisa huko, kama ilivyo katika tafsiri ya Ibnu Jarir, Ibnu Mundhir na Ibnu Aby Hatim. Na namna hivi ndivyo alivyofasiri Sayyidna Abubakrinis Siddiq na akawataka watu waabudu hivi, kama walivyotaja haya ulamaa wa Hadithi hawa: Ibnu Aby Shayba, Ibnu Mundhir, Ibnu Aby Hatim, Abu Nuaym, Al Hakim na Al Bayhaqy, kama ilivyo katika sahifa 413 ya Juzuu ya tatu ya tafsiri ya Imam Ash Shawkany inayoitwa *Fat-hul-Qadyr*.

94. Inatosha Aya hii kupinga maneno ya upuuzi yanayoandikwa na baadhi ya watu wanaothubutu kujita wanavyuoni. Wanasadiki kuwa Mwislamu mwanaharamu hataingia Pepo ya Mwenyezi Mungu aliyowaekea Waislamu wema, lakini wataingia Pepo ya Shaddad. Mwislamu mwenye kujua, kidogo tu hivi haiwi kwake kusadiki haya, seuze anayejiita Mwanachuoni. Hakuna katika Qurani wala Hadithi SAHIHI za mtume habari ya kuwa Mwanaharamu ataingia Pepo ya Shaddad.

95. Na ni haramu (haiwi) kwa (watu wa) mji tuliouangamiza ya kwamba wao hawatarejea (kwetu).

96. Hata watakapofunguliwa Yaajuj na Maajuj wakawa wanateremka kutoka kila mlima (hapo Kiama kitakuwa tayari).

97. Na itafika ile ahadi ya haki. Hapo ndipo yatakodoka macho ya wale waliokufuru (wakisema): "Ole wetu! (Ee adhabu yetu!) Bila shaka tulikuwa katika mughafala na (Jambo) hili, bali tulikuwa madhalimu (wa nafsi zetu)."

98. Hakika nyinyi na wale mnaowaabudu, mkamwacha Mwenyezi Mungu, ni kuni za Jahanamu; nanyi mtaifikia (hiyo Jahanamu mkae humo).

99. Lau hawa wangalikuwa miungu wasinge ifikia (hiyo Jahanamu). Na wote humo watakaa milele.

100. Wao humo watapiga kelele, nao humo hawatasikia (la kuwaliwaza).

101. Hakika hao ambao wema wetu umewafikia, hao watakuwa mbali nayo (hiyo Jahanamu)

102. Hawatausikia (hata) mvumo wake, nao watakua milele katika yale yanayoyatamani nafsi zao.

103. Hautawahuzunisha huo mtaharuki mkubwa, na Malaika watawapokea (na kuwaambia): "Hii ndiyo ile siku yenu mliyokuwa mkiahidiwa."

104. Siku tutakapozikunja mbingu kama mkunjo wa karatasi za maandishi. Kama tulivyoanza umbo la awali tutalirudisha tena. Ni ahadi iliyo juu yetu, bila shaka sisi ni wenye kufanya (tuyasemayo).

105. Na nakika tuliandika katika Zaburi baada ya (kuandika katika) *Allawhul Mahfudh* ya kwamba ardhi (hii) watairithi waja wangu walio wema.

106. Hakika katika haya pana mawaidha (ya kutosha) kwa watu wafanyao ibada.

وَحَرَّمَ عَلَىٰ قَرِيَّةٍ أَهْلَكْنَاهَا إِنَّهُمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿١٥﴾

حَتَّىٰ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ وَهُمْ مِنْ كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ ﴿١٦﴾

وَاقْتَرَبَ الْوَعْدُ الْحَقُّ فَإِذَا هِيَ شَاخِصَةٌ أَبْصَارُ الَّذِينَ كَفَرُوا يَوِيلْنَا قَدْ كُنَّا فِي عَفْوَةٍ مِنْ هَذَا بَلْ كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿١٧﴾

إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ أَنتُمْ لَهَا وَرِدُونَ ﴿١٨﴾

لَوْ كَانَ هَؤُلَاءِ آلِهَةً مَا وَرَدُّوهُمْ وَلَا يَخَافُهُمْ خَلِدُونَ ﴿١٩﴾

لَهُمْ فِيهَا زَوْجٌ وَهُمْ فِيهَا لَا يَسْمَعُونَ ﴿٢٠﴾

إِنَّ الَّذِينَ سَبَقَتْ لَهُمْ مِنَّا الْحُسْنَىٰ أُولَٰئِكَ عَنْهَا مُبْعَدُونَ ﴿٢١﴾

لَا يَسْمَعُونَ حَسِيسَتِهَا وَهُمْ فِي مَا اشْتَهَتْ أَنفُسُهُمْ خَلِدُونَ ﴿٢٢﴾

لَا يَحْزَنُهُمُ الْفَزَعُ الْأَكْبَرُ وَتَتَلَقَّوهُمُ الْمَلَائِكَةُ هَذَا يَوْمُكُمْ الَّذِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٢٣﴾

يَوْمَ نُطَوِّعُ السَّمَاءَ كَطَيِّ السِّجْلِ لِكُتُبِكُمْ كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ يُعِيدُهُ وَعَدَّا عَلَيْنَا وَإِنَّا كُنَّا فاعِلِينَ ﴿٢٤﴾

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ ﴿٢٥﴾

إِنَّ فِي هَذَا لَبَلَاغًا لِقَوْمٍ غَابِرِينَ ﴿٢٦﴾

96. Wamepachika katika hii Aya waliyoifanya kuwa ya 97 maneno haya:— "Na ya 97 inaonyesha ya kuwa hata Yaajuj na Maajuj (Gog na Magog), juu ya kufanikiwa kwao katika mambo ya kidunia, hawataweza kuwarejesha waliokufa." Wametia haya ili kuzidi kugongomelea maneno ya kuwa Nabii Isa hatarejea ulimwenguni. Wao wanasema hata kina Yaajuj hawawezi jambo hilo. Lakini sisi hatusemi kuwa jambo hilo la kumleta Nabii Isa atalifanya binaadamu. Atalifanya Mwenyewe Mwenyezi Mungu kama alivyotwambia Mtumewe.

105, 106. Tukilifasiri tamko la ardhi lililomo katika Aya ya 105 kwa Pepo — kama walivyofasiri ulamaa wengineo — basi Aya hizi zitazidi kutia nguvu yale tuliyoyasema katika Aya ya 95.

107. Nasi hatukukutuma, (hatukukuleta) ila uwe rehema kwa walimwengu (wote).

108. Sema: "Sikuletewa Wahyi (Sikufunuliwa), ila kwamba Mungu wenu ni Mungu mmoja tu. Je! Murnesilimu?"

109. Na kama wakigeuka, basi sema: "Nime kutangazieni sawasawa, wala sijui yako karibu au mbali yale mliyoahidiwa."

110. Hakika yeye anajua kauli iliyo dhahiri na anajua mnayoyaficha.

111. Wala sijui kama hii ni fitina kwenu na starehe mpaka muda kidogo (au nini).

112. Akasema: "Mola wangu! Hukumu kwa haki." Na Mola wetu ndiye Mwenye rehema, Aombwaye msaada juu ya hayo mnayoyasema.

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٠٧﴾

قُلْ إِنَّمَا يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُمُ إِلَهٌ وَاحِدٌ،  
فَهَلْ أَنْتُمْ مُّسْلِمُونَ ﴿١٠٨﴾


فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُلْ آذَنْتُكُمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ وَإِنْ  
آذَرْتُمِي أَقْرَبُ بِكُمْ مِّمَّا تُوعَدُونَ ﴿١٠٩﴾

إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ مِنَ الْقَوْلِ وَيَعْلَمُ مَا كَلَّمْتُمُونَ ﴿١١٠﴾

وَإِنْ آذَرْتُمِي لَعْنَةُ اللَّهِ، فَثِنَّةٌ لَّكُمْ وَمَتَاءٌ لِّي  
حَيْثُ ﴿١١١﴾

قُلْ رَبِّ احْكُم بِالْحَقِّ، وَرَبُّنَا الرَّحْمَنُ  
الَّذِي السُّعْتَانُ عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ ﴿١١٢﴾

107. Mitume waliotangulia kabla ya Mtume Muhammad s.a.w., kila mmoja alipelekwa kwa kabila yake na taifa lake tu. Mtume Muhammad s.a.w. peke yake ndiye aliyepewa utukufu wa kupelekwa kwa watu wote.



SURATUL HAJJ

(Imeteremku Madina)

Ina Makara 10

Ina Ayu 78

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Enyi watu! Mcheni Mola wenu, hakika mtetemeko wa Kiama ni jambo kubwa (kabisa).

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ: إِنَّ زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيمٌ ①

2. Siku mtakapokiona (hicho Kiama) — kila mwanamke anyonyeshaye atamsahau amnyonyeshaye, na kila mwenye mimba ataizaa mimba yake (kabla ya wakati kufika). Na utawaona watu wamelewa; kumbe hawakulewa, lakini ni adhabu ya Mwenyezi Mungu (tu hiyo) iliyo kali.

يَوْمَ تَرُؤْنَهَا تَذْهَلُ كُلُّ مُرْضِعَةٍ عَمَّا أَرْضَعَتْ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمْلٍ حَمْلَهَا وَتَرَى النَّاسَ سُكَرَىٰ وَمَا هُمْ بِسُكَرَىٰ وَلَٰكِنَّ عَذَابَ اللَّهِ شَدِيدٌ ②

3. Na katika watu wako wanaobishana juu ya Mwenyezi Mungu pasipo ilimu, na wanamfuata kila shetani asi.

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَيُبْغِيهِ كُلُّ شَيْطَانٍ مُّرِيدٍ ③

4. Ameandikiwa (huyo shetani) ya kwamba atakayemfanya kuwa rafiki, basi kwa yakini yeye atampoteza na kumuongoza katika adhabu ya Moto mkali.

كَتَبَ عَلَيْهِ أَنَّهُ مَن تَوَلَّاهُ فَأَنَّهُ يُضِلُّهُ وَ يَهْدِيهِ إِلَىٰ عَذَابِ السَّعِيرِ ④

5. Enyi watu! Kama mumo katika shaka juu ya ufufuo; (mnaona haimkiniki kufufuliwa), basi (tazameni namna tulivyokuumbeni): kwa hakika tulikuumbeni kwa udongo. (Mzee wenu Nabü Adamu), kisha (tukawa tunakuumbeni nyinyi) kwa manii, (mbegu ya uhai), kisha (yanageuka) kuwa kipande cha damu, kisha huwa kipande cha nyama kinachoumbika, (kinachofanyika sura) na kisichoumbika; ili tukubainishieni (Kudra yetu). Nasi tunakikalisha matumboni tunachokitaka mpaka muda uliowekwa, kisha tunakutoeni kwa hali ya utoto; kisha (tunakuleeni) ili mfikie balebhe yenu. Na kuna wanaokufa (kabla ya kufikilia hali hii). Na katika nyinyi wako wanaorudishwa katika umri dhalili; asijue chochote baada ya kule kujua kwake, na unaiona ardhi imetulia kimya lakini tunapoyateremsha maji juu yake, inataharaki na kukuwa na kuotesha kila namna ya mimea mizuri.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِن كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّنَ الْبَعْثِ فَإِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِّن نَّبَاتٍ مِّن نُّطْفَةٍ ثُمَّ مِّن نُّطْفَةٍ ثُمَّ مِّن عَلَقَةٍ ثُمَّ مِّن مَّضْغَةٍ مُّخَلَّفَةٍ وَغَيْرِ مُخَلَّفَةٍ لِتُبَيِّنَ لَكُمْ وَنُقِرُّ فِي الْأَرْحَامِ مَا نَشَاءُ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَدَّدٍ ثُمَّ نُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ إِن تَبْلُغُوا أَشُدَّكُمْ، وَمِمَّن مِّن مَّن يَتُوبُ وَ مِمَّن مِّن مَّن يَئُودُ إِلَىٰ أَرْدَلِ الْعُمُرِ لِكَيْلَا يَعْلَمَ مِن بَعْدِ عِلْمٍ شَيْئًا. وَتَرَكَ الْأَرْضَ هَامِدَةً فَإِذَا أَنزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَتْ وَأَنْبَتَتْ مِن كُلِّ زَوْجٍ بَهِيجٍ ⑤

5. Mtu aliye na shaka ya kufufuliwa anatakiwa azingatie yaliyomo katika Aya hii tukufu ajione alikotoka na alikofika. Kisha atazame Ardhi inavyokufa kwa chaka na kufufuliwa kwa mvua ili ajuwe kwamba Aliyeweza kufanya hayo, hapana linalomshinda.

6. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu yuko, na kwamba Yeye huwahuisha wafu, na kwamba Yeye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu

7. Na kwamba Kiama kitakuja, hapana shaka ndani yake; na kwa hakika Mwenyezi Mungu atawafufua walio makaburini.

8. Na katika watu wako wanaojadiliana juu ya Mwenyezi Mungu bila ilimu wala uwongozi wala Kitabu chenye nuru.

9. Wageuzao shingo zao ili kupoteza (watu) katika njia ya Mwenyezi Mungu. Watapata fedheha duniani na tutamwonjesha (kila mmoja katika wao) siku ya Kiama adhabu ya kuungua (na kumwambia:)

10. "Hii ni kwa sababu ya yale iliyotanguliza mikono yako, (mwili wako). Na bila shaka Mwenyezi Mungu si dhalimu kamwe kwa waja wake."

11. Na katika watu wako wanaomuabudu Mwenyezi Mungu ukingoni. Ikiwafikia kheri, hutulia kwayo, na ikiwafikia fitina, (msukosuko), hubwatika juu ya uso wake (akasunukia, hataki kuuona tena huo Uislamu). Amepata hasara ya dunia na Akhera; hiyo ndiyo khasara iliyo dhahiri.

12. Wanawaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, wasiowadhuru (wakiacha kuwaabudu) wala wasiowafaa, (wanapowaabudu). Huo ndio upotofu ulio mbali kabisa (na haki).

13. Wanawaomba wale ambao bila shaka dhara yao i-karibu zaidi kuliko nafuu yao. Kwa yakini (hao wanaowaabudu badala ya Mungu) ni walinzi wabaya na ni rafiki wabaya (wasiokuwa na maana yoyote).

8. Panakatazwa kwa ukali mkubwa kushindana katika mambo ya dini pasina ilimu ya dini. Na ilimu sahihi ya kujua dini ni ile iliyomo katika Qurani na Hadithi za Mtume zilizo sahihi na iliyomo katika vitabu vya dini vya kutegemewa vilivyokubaliwa; siyo kila kitabu tu.

Na yasiyokuwa ya dini pia ukishindana shindana kwa ilimu. Huna ruhusa KULISADIKI lolote pasina kujua yakini yake, kama anavyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 36 ya Surat Bani Israil na nyinginezo zilizomo ndani ya Qurani; na kama anavyosema Mtume katika Hadithi zake.

11. Tumeletwa ulimwenguni tufanyiwe mitihani ili tusafike barabara kabla ya kwenda Akhera; kama inavyosafishwa dhahabu kwa kutiwa motoni. Basi natuvumilie na tushike hayo tuliyoambiwa na Mwenyezi Mungu na Mtumewe. Na kila namna: Baada ya Dhiki ni Faraji tu. Tusikate tamaa lakini tupanie barabara katika kujitenga na hizo balaa zisitufikilie, na zikitufikia tustahamili, na huku tunajitatua nazo kwa mwisho wa uweza wetu: NA KUMUOMBA Mwenyezi Mungu. Siyo kuomba Mizimu na Mapepo na Makaburi; kama tulivyobainishiwa katika Aya ya 12 kuwa hawawezi kunufaisha wala kuondosha madhara.

Mambo yote ni ya Mungu: Atakalo ndilo huwa. Ndiye Pweke mwenye quwa: Mwenye amri na shani.

ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنََّّهُ يُخَيِّمُ الْمَوْتَىٰ  
وَأَنَّ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٦﴾

وَأَنَّ السَّاعَةَ آتِيَةٌ لَّارْتَيْبٍ فِيهَا ۖ وَأَنَّ اللَّهَ يَبْعَثُ مَنْ فِي الْقُبُورِ ﴿٧﴾

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ  
عِلْمٍ وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُّنبِئٍ ﴿٨﴾

ثَانِي عَطْفِهِ يُضِلُّ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ۗ لَهُ فِي  
الدُّنْيَا خِزْيٌ وَنَذِيقُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَذَابَ  
الْحَرِيقِ ﴿٩﴾

ذَلِكَ بِمَا قَدَّمْت يَدَكَ ۖ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلَّامٍ  
لِّلْعَبِيدِ ﴿١٠﴾

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقْبُدُ اللَّهَ عَلَىٰ حَرْفٍ ۖ فَإِن  
أَصَابَهُ خَيْرٌ اطْمَأَنَّ بِهِ ۚ وَإِن أَصَابَتْهُ  
فِتْنَةٌ ائْتَلَبَ عَلَيْهَا وَجْهَهُ خَسِرَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةَ ۗ  
ذَلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ ﴿١١﴾

يَدْعُوا مَن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُ وَمَا  
يَنْفَعُهُ ۗ ذَلِكَ هُوَ الضَّلُّ الْبَعِيدُ ﴿١٢﴾

يَدْعُوا لِمَن صَرَفَ أَقْرَبُ مِن نَّفْعِهِ ۗ لَيْسَ  
الْمَوْلَىٰ وَلَيْسَ الْعَشِيرُ ﴿١٣﴾

14. Bila shaka Mwenyezi Mungu atawaingiza wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, katika mabustani (Pepo) yapitayo mito mbele yake. Hakika Mwenyezi Mungu hufanya atakavyo.

15. Anayedhani ya kwamba Mwenyezi Mungu hatamnusuru, (hatamsaidia Mtume) katika dunia na Akhera, basi naafunge kitanzi juu, kisha ajinyonge (kama hataki kuyaona hayo). Na atazame: Je! Hila yake yaweza kuyaondoa yale yaliyomghadhibisha?

16. Na namna hivi tumeiteremsha (Qurani) kuwa maneno yaliyo wazi; na bila shaka Mwenyezi Mungu humuongoza amtakaye.

17. Hakika wale walioamini, na ambao ni Mayahudi na Wasabai na Wakristo na Majusi na wale washirikishao, kwa yakini Mwenyezi Mungu atahukumu baina yao siku ya Kiama. Hakika Mwenyezi Mungu ni Shahidi juu ya kila kitu.

18. Je! Huoni ya kwamba Mwenyezi Mungu kinamsujudia kila kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini na jua na mwezi na nyota na milima na miti na wanyama na wengi miongoni mwa watu? Na wengi (pia) imewalazimu adhabu (ya Mwenyezi Mungu). Na ambaye Mwenyezi Mungu amemfedhehesha, basi hakuna atakayempa hishima. Kwa yakini Mwenyezi Mungu hufanya apendayo.

19. Hawa mahasimu wawili waliohasimiana kwa ajili ya Mola wao. Basi wale waliokufuru watakatiwa nguo za Moto na yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji yachemkayo.

20. Kwa (maji) hayo vitayayushwa vilivyomo matumboni mwao na ngozi zao (pia).

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ يُدْخِلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ذَٰلِكَ اللَّهُ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ ﴿١٥﴾

مَنْ كَانَ يَكُنْ أَنْ لَنْ يَنْصُرَهُ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ فَلْيَمْدُدْ بِسَبَبٍ إِلَى السَّمَاءِ ثُمَّ لِيَقْطَعْ فَلْيَنْظُرْ هَلْ يُدْهِبُ كَيْدَهُ مَا يَكْفِيهِ ﴿١٥﴾

وَكَذَٰلِكَ أَنْزَلْنَاهُ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ ۖ وَأَنَّ اللَّهَ يَهْدِيَ مَن يَشَاءُ ﴿١٥﴾

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالضَّالِّينَ وَالنَّاصِرِينَ وَالْمُجْرِمِينَ وَالَّذِينَ اشْرَكُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿١٥﴾

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَخْتِجُ لَهٗ مَن فِي السَّمٰوٰتِ وَمَن فِي الْأَرْضِ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ وَالنُّجُومُ وَالْجِبَالُ وَالشَّجَرُ وَالدَّوَابُّ وَكَثِيرٌ مِّنَ النَّاسِ وَكَثِيرٌ حَقَّ عَلَيْهِ الْعَذَابُ ۗ وَمَن يُهِنِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِن مُّكْرِمٍ ۗ إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ﴿١٥﴾

هٰذِهِ حَصْمِيْنَ اٰخَصَّوْا فِي رَيْبِهِمْ ذَا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا قَطَعَتْ لَهُمْ ثِيَابٌ مِّنْ سَآءِ يَوْمٍ مِّنْ قَوْفٍ رُّؤْسِهِمُ الْحَمِيْمُ ﴿١٩﴾

يُصْهَرُ بِهَا فَا فِي بُصُوْنِهِمْ وَالْجُلُوْدُ ﴿٢٠﴾

الْحَمِيْمُ

15. Wanakatishwa tamaa makafiri; wanaambiwa kuwa Mtume atanusurika tu; Na wa kuhizika ni wao. Anayekwenda kinyume na Mungu atahizika tu; ikiwa si duniani, basi akhera; au kote.

19. Aya hii, khasa inawakhusu wale Waislamu wa mwanzo, (Ahli Badr) waliokabiliana na hao makafiri wa mwanzo waliokabiliana na Waislamu. Na khasa wale Waislamu watatu wa mwanzo kabisa waliosimama kupigana na makafiri watatu wa mwanzo waliotoka ili wakabiliane mwanzo na Waislamu. Waislamu hao ni:

- (a) Sayyidna Ali bin Abi Talib bin Abdul Muttalib bin Hashim bin Abd Manaf — Alikabiliana na Walid bin Utba bin Rabia bin Abd Shams bin Abd Manaf. AKAULIWA WALID.
- (b) Sayyidna Hamza bin Abdul Muttalib bin Hashim bin Abd Manaf — Alikabiliana na Shayba bin Rabia bin Abd Shams bin Abd Manaf. AKAULIWA SHAYBA.
- (c) Sayyidna Abu Ubeyda bin Harith bin Abdul Muttalib bin Abd Manaf—Alikabiliana na Utba bin Rabia bin Abd Shams bin Abd Manaf. WAKAUWANA.

Pale pale alikufa Utba na baadaye akafa Sayyidna Abu Ubeyda.

Basi na kila watakaopigania haki au batili yatawafika haya na kama haya na zaidi. Wema yatawafika yaliyomo katika Aya ya 23. Na wabaya yatawafika yaliyo katika Aya ya 19, 20, 21 na 22.

21. Na kwa ajili yao (yatakuwapo) marungu ya chuma.

22. Kila mara watakapotaka kutoka humo (adhabuni) kwa sababu ya uchungu, (maumivu) watarudishwa mumo humo na (kuambiwa): "Ionjeni adhabu ya kuungua."

23. Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza wale walioamini na kufanya vitendo vizuri (katika) mabustani yapitayo mito mbele yake. Humo watavishwa mapambo ya mikononi ya dhahabu na lulu, na mavazi yao humo yatakuwa hariri.

24. Na wataongozwa (kwenda mahala) kwenye maneno mazuri na kuongozwa katika njia ya (Pepo ya Mwenyezi Mungu). Mwenye kuhimidiwa.

25. Hakika wale waliokufuru (wenyewe) na wakawazuilia (wengine) njia ya Mwenyezi Mungu na (wakawazuilia kuingia) Msikiti uliotukuzwa ambao tumeufanya kwa ajili ya watu wote sawasawa, kwa wakao humo na wageni; (watu hao tutawaadhibu adhabu kali). Na kila atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhuluma basi tutamuonjesha adhabu iumizayo.

26. Na (kumbuka) tulipomkalisha Ibrahimu mahali penye ile Nyumba (takatifu na tukamwambia): "Usinishirikishe na chochote na isafishe Nyumba yangu kwa ajili ya waizungukao na wanaokaa hapo (kufanya ibada yao) na wanaorukuu na kusujuduu, (wanaosali)."

27. Na (tukamwambia): "Utangaze kwa watu habari za Hija, watakujiia, (wengine) kwa miguu na (wengine) juu ya kila mnyama aliyekonda (kwa machofu ya njiani wakija kutoka katika kila njia ya mbali;

28. Ili washuhudie manufaa yao na (ili wakithirishe) kulitaja jina la Mwenyezi Mungu—katika siku zinazojulikana (fadhila zake)—juu ya yale aliyowaruzuku, nao ni wanyama wenye miguu minne. Na kuleni katika wanyama hao na mlisheeni mwenye shida aliyefakiri.

29. Kisha wajisafishe taka zao, na watimize nadhiri zao, na waizunguke Nyumba ya Kale, (Nyumba kongwe—Al-Kaaba)."

وَلَهُمْ مَقَامٌ مِّنْ حَدِيثِكُمْ ۝١١

كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ يَخْرُجُوا مِنْهَا مِنْ غَمٍّ أُعِيدُوا  
فِيهَا وَذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ۝١٢

إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ  
جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ يُحَلَّوْنَ فِيهَا  
مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا  
خَرِيرٌ ۝١٣

وَهَذَا إِلَى الطَّيِّبِ مِنَ الْقَوْلِ: وَهَذَا إِلَى  
صِرَاطِ الْحَمِيدِ ۝١٤

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ  
وَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ الَّذِي جَعَلْنَاهُ لِلنَّاسِ  
سَوَاءً الْعَاكِفُ فِيهِ وَالْبَادِ وَمَنْ يُرِدْ فِيهِ  
بِالْحَادِ بِظُلْمٍ نُّذِقْهُ مِنْ عَذَابِ الْعَذَابِ ۝١٥

وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَاهِيمَ مَكَانَ الْبَيْتِ أَنْ لَا  
تَشْرِكْ بِي شَيْئًا وَطَهِّرْ بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ  
وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ۝١٦

وَإِذْ فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ يَاأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَى  
كُلِّ مَضَامِيرٍ ثِيَابٍ مِّنْ كُلِّ نَجْدٍ عَمِيْقٍ ۝١٧

لِيَشْهَدُوا مَنَافِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ فِي  
أَيَّامٍ مَّعْلُومَاتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُمْ مِّنْ بَهِيمَةٍ  
الْأَنْعَامِ فَكُلُوا مِنْهَا وَأَطِعُوا الْبَآئِسَ الْفَقِيرَ ۝١٨

ثُمَّ لِيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلِيُؤْتُوا نُذُورَهُمْ وَلِيَطَّوَّفُوا  
بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ ۝١٩

23. Kwa hima yao makadiyani ya kutaka kumpinga tu Mwenyezi Mungu hupenyeza upotofu wao hata pasipopenyezeka. Kama katika Aya hii waliyoifanya kuwa ya 24. Aya hii ni dhahiri kuwa inataja habari za akhera, wao wanazifanya za kiduniani. Wakatia farumu ya bure ambayo hapo sipo mahala pake.

29: Kabla ya Uislamu. Waarabu walikuwa wakitukuza Al-Kaaba. Na kwa ilivyokuwa ni jengo la zamani sana

30. Namna hivi iwe; Na anayevitukuza vitu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu, basi (kufanya) hivyo ni kheri yake mwenyewe mbele ya Mola wake. Na mumehalalishiwa wanyama isipokuwa waie mnaosomewa humu (katika Qurani kuwa wasiliwe); Basi jiepusheni na uchafu wa masanamu na jiepusheni na usemi wa uwongo.

31. Mkhalisike kwa Mwenyezi Mungu, bila kumshirikisha. Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu ni kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, kisha ndege wakamnyakua au upepo kumtupa mahali pa mbali.

32. Namna hivi; anayezihishimu alama za (dini ya) Mwenyezi Mungu, basi hilo ni jambo la katika utawa (ucha Mungu) wa nyoyo.

33. Katika (wanyama) (mnaowapeleka Makka kuchinjwa) mnayo (ruhusa kutumiya) manufaa (yake) mpaka muda maalumu: (Nao ni hapo inapopasa kuchinjwa). Kisha mahali pa kuchinjwa kwake ni (karibu na) ile Nyumba kongwe ya Kale.

34. Na kila uma tumewafanyia mahali pa kuchinjia mihanga ya Ibada ili kulitaja jina la Mwenyezi Mungu juu ya vile alivyowaruzuku katika wanyama hao wenye miguu mine. Basi Mungu wenu ni Mungu mmoja tu; Jinyenyekesheni kwake. Na waambie khabari njema wale wanyenyekavu.

35. Ambao, anapotajwa Mwenyezi Mungu, nyoyo zao hutetemeka, na wanaovumilia juu ya yale yanayowasibu na wanasimamisha Sala na katika vile tulivyowapa wanatoa.

36. Na ngamia (na ng'ombe na mbuzi na kondoo wa sadaka) tumekufanyieni kuwa katika alama za (dini ya) Mwenyezi Mungu; kwa hao mnayo kheri (nyingi). Basi litajeni jina la Mwenyezi Mungu juu yao wasimamapo safu safu (mnawachinja); Na waangukapo ubavu, kuleni katika hao na mlishe makafiri wanaoomba na wanaorondearondea bila ya kuomba. Namna hivi tumewatiisha kwa ajili yenu ili mpate kushukuru.

37. Nyama zao (wanyama hao wanaochinjwa) hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini

ذٰلِكَ وَمَنْ يُعْظِمِ حُرْمَتِ اللّٰهِ فَهُوَ خَيْرٌ لِّهٖ  
عِنْدَ رَبِّهِ ۚ وَ اُحِلَّتْ لَكُمْ الْاَنْعَامُ اِلَّا مَا يَتْلُو  
عَلَيْكُمْ فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْاَوْثَانِ  
وَاجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ ﴿٣٠﴾

حُنْفَاءٌ لِلّٰهِ غَيْرَ مُشْرِكِيْنَ بِهِ ۚ وَمَنْ  
يُشْرِكْ بِاللّٰهِ فَكَانَ لِنَارٍ مِّنَ السَّمَآءِ قَتْلًا  
ظَلِيْمًا ۗ اَوْ تَهْوٰى بِهٖ الرِّيْبِ فِيْ مَكَانٍ  
سَّجِيۡتٍ ﴿٣١﴾

ذٰلِكَ ۚ وَمَنْ يُعْظِمِ شَعَائِرَ اللّٰهِ فَاِنَّهَا مِنْ تَقْوٰى  
الْقُلُوْبِ ﴿٣٢﴾

لَكُمْ فِيْهَا مَنَافِعٌ اِلَىٰ اَجَلٍ مُّسَمًّى ثُمَّ مَحِلُّهَا  
اِلَى الْبَيْتِ الْعَتِيْقِ ﴿٣٣﴾

وَرِكْلِۙ اُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنَسْكَ لِيّٰذِكُرُوا اللّٰهَ  
عَلٰٓى مَا رَزَقْتَهُمْ مِّنْ بَهِيمَةِ الْاَنْعَامِ ۗ فَالْهٰكُمُ  
اِلٰهٌ وَّاحِدٌ فَلَاۤ اَسْلُوْا ۗ وَكَبِّرْ  
الْمُحِبِّيْنَ ﴿٣٤﴾

الَّذِيْنَ اِذَا ذُكِرَ اللّٰهُ وُجِئَتْ قُلُوْبُهُمْ  
وَالصُّبْحِيْنَ عَلٰٓى مَاۤ اَصَابَهُمْ وَالْمُغِيْبِيْنَ  
الصَّلٰوةِ ۗ وَمِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ﴿٣٥﴾

وَالْبُدْنَ جَعَلْنٰهَا لَكُمْ مِّنْ شَعَائِرِ اللّٰهِ لَكُمْ  
فِيْهَا خَيْرٌ ۗ فَاذْكُرُوا اللّٰهَ عَلَيْهَا صَوَآتٍ ۗ  
فَاِذَا وَجَبَتْ جُنُوْبُهَا فَكُلُوْا مِنْهَا وَاَطْعِمُوْا  
الْقَاۡنِعَ وَالْمِعْتَرَةَ ۗ كَذٰلِكَ سَخَّرْنٰهَا لَكُمْ  
لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿٣٦﴾

لَنْ يَبْتٰلَ اللّٰهُ لِحَوْمِهَا وَلَا دِمَآؤِهَا وَلٰكِنْ

waliita *Al-Baytul Atiq* yaani Nyumba ya Kale. Si chini kuliko miaka 6,000 tangu kujengwa na Nabii Ibrahimu na Nabii Ismaili. Ama kule kusema kuwa imejengwa na Malaika au Nabii Adamu: siyo kauli yenye nguvu.

inamfikia (kwake Mwenyezi Mungu) taa, (Utawa) yenu. Namna hivi tumewatiisha kwenu, ili mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa sababu ya huku kukuongozeni. Na wape khabari njema wafanyao mema.

38. Hakika Mwenyezi Mungu huwakinga wale walioamini. Bila shaka Mwenyezi Mungu hampendi kila haini, asiyeshekuru.

39. Wameruhusiwa (kupigana) wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa. Na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia;

40. Ambao wametolewa majumbani, (mjini) mwao pasipo haki ila kwa sababu wanasema: "Mola wetu ni Mwenyezi Mungu." Na kama Mwenyezi Mungu asingaliwakinga watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisa na nyumba nyengine za ibada na misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu hutajwa kwa wingi. Na bila shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anayesaidia dini yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda.

41. Wale ambao tukiwamakinisha, (tukiwaweka uzuri) katika ardhi husimamisha Sala na wakatoa Zaka na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mabaya. Na marejeo ya mambo ni kwa Mwenyezi Mungu.

42. Na kama wakikukadhibisha (hawa makafiri wa zama zako, hapana ajabu) kwani walikadhibisha kabla yao watu wa Nuhu na kina Adi na kina Thamudi.

43. Na watu wa Ibrahimu na watu wa Luti.

44. Na watu wa Madyan. Na Musa pia alikadhibishwa. Nikawapa muda makafiri kisha nikawatia mkononi. Basi ilikuwaje adhabu yangu!

45. Miji mingapi tuliangamiza iliyokuwa ikidhulumu, ikaanguka juu ya mapaa yake; na visima (vingapi) vilivyoachwa, na majumba (yaliyokuwa) madhubuti?

46. Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate nyoyo, (akili) za kufahamia, au masikio ya kusikilia? Kwa hakika macho hayapofoki (yakadhuru katika

يَنَالُهُ التَّقْوَىٰ مِنكُمْ كَذَلِكَ سَخَّرَهَا لَكُمْ لِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَيْكُمْ وَلِيُبَشِّرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٨﴾

إِنَّ اللَّهَ يُدْفِعُ عَنِ الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ خَوَّانٍ كَفُورٍ ﴿٣٩﴾

أَذِنَ لِلَّذِينَ يُقْتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظَلَمُوا وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ ﴿٤٠﴾

الَّذِينَ أَخْرَجُوا مِنَ دْيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّا أَنْ يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّهُ، وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَهَدَمَتْ صَوَامِعُ وَبِيَعٌ وَصَلَوَاتٌ وَ مَسَاجِدُ يُذَكَّرُ فِيهَا اسْمُ اللَّهِ كَثِيرًا، وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَن يَنْصُرُهُ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٤١﴾

الَّذِينَ إِنْ مَكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَآمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ، وَاللَّهُ عَاقِبَةُ الْأُمُورِ ﴿٤٢﴾

وَإِنْ يَكْفُرْ بِكَ فَكُفِّرْ بَدَلَهُمْ فَإِن كَدَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمٌ نَّوْجٌ وَعَادٌ وَثَمُودٌ ﴿٤٣﴾

وَ قَوْمِ إِبْرَاهِيمَ، وَ قَوْمِ لُوطٍ ﴿٤٤﴾

وَ أَصْحَابِ مَدْيَنَ، وَ كَذَّبَ مُوسَىٰ فَأَمَلَيْتُ لِلْكَافِرِينَ ثُمَّ أَخَذْتُهُمْ، فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٤٥﴾

فَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ أَهَكَّكْنَاهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ فَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا وَبِيْرٌ مُّعْطَلَةٌ وَ قَصْرِ مَشِيدٍ ﴿٤٦﴾

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَتَكُون لَهُمْ قُلُوبٌ يَعْقِلُونَ بِهَا أَوْ آذَانٌ يَسْمَعُونَ بِهَا، فَإِنَّهَا لَا

39. Waislamu waliishi Makka muda wa myaka kumi na tatu, wakiadhibiwa kwa adhabu zisizostahamilika. Na juu ya hayo hawakupewa ruhusa ya kujitetea. Na mwisho wakapewa amri ya kutupa watani wao, mali yao na watu wao, wahamie Madina. Huko ndiko ilikoshuka Aya hii kuwapa ruhusa ya kujitetea.





dini), lakini nyoyo ambazo zimo vifuani ndizo zinazopofoka (zikadhuru katika dini).

47. Na wanakuhimiza ulete adhabu, lakini Mwenyezi Mungu hatavunja ahadi yake (aliyoweka ya kuwa adhabu ya kweli kweli itakuwa akhera); na kwa hakika siku moja kwa Mola wako ni kama myaka elfu mnavyohisabu nyiye (nyinyi).

48. Na (watu wa) miji mingapi niliyowapa muda; na hali walikuwa wakidhulumu? Kisha niliwatia mkononi; na kwangu ndiko marudio (yote).

49. Sema: "Enyi watu! Bila shaka mimi kwenu ni Mwonyaji niliye dhahiri."

50. Basi wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri watapata msamaha na riziki (tukufu) zenye hishima.

51. Na wale wanaojitahidi kuzipinga Aya zetu hao ndio watu wa Motoni.

52. Na hatukumtuma kabla yako Mtume mwenye kupewa Kitabu wala Mtume asiyepewa Kitabu chake makhsusi (lakini anafuata Kitabu cha Mtume aliyemtangulia), ila anaposoma, Shetani hutia (fitina) katika masomo yake hayo. Lakini Mwenyezi Mungu huondoa anayoyatia Shetani, kisha Mwenyezi Mungu huzimakinisha Aya zake; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima

53. (Hufanyika haya) ili alifanye—lile analotia Shetani—kuwa mihani kwa wale wenye maradhi nyoyoni mwao na ambao nyoyo zao ni ngumu. Na bila shaka madhalimu wamo katika khitilafu iliyo mbali (na haki)

54. Na ili wajue wale waliopewa ilimu ya kwamba hiyo ni haki iliyotoka kwa Mola wako na waiamini, na ili zinyenyekee kwake nyoyo zao. Na kwa yakini Mwenyezi Mungu ndiye awaongozaye wale walioamini katika njia iliyonyoka.

تَعْنَى الْإِبْصَارِ وَلَكِنْ تَعْنَى الْقُلُوبِ الَّتِي فِي الصُّدُورِ ﴿٥٧﴾

وَيَتَّبِعُونَكَ بِالْعَدَابِ وَكَانَ يُخْلِفُ اللَّهُ وَعْدَهُ، وَإِنَّ يَوْمًا عِنْدَ رَبِّكَ كَأَلْفِ سَنَةٍ مِمَّا تَعُدُّونَ ﴿٥٨﴾

وَكَانَ مِنَ قَرِيْبَةٍ أَمْكَيْتَ لَهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ ثُمَّ أَخَذَتْهَا، وَإِلَى الْمَصِيْرِ ﴿٥٩﴾  
قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ يُدِيرُ الْغُيُوبَ ﴿٦٠﴾

فَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٦١﴾

وَالَّذِينَ سَعَوْا فِي آيَاتِنَا مُعْجِزِينَ أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿٦٢﴾

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ وَلَا نَبِيٍّ إِلَّا إِذَا تَمَنَّى أَلْقَى الشَّيْطَانُ فِي أُمْنِيَّتِهِ، فَيَلْسَنُ اللَّهُ مَا يُلْقِي الشَّيْطَانُ ثُمَّ يُحْكِمُ اللَّهُ آيَاتِهِ، وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٣﴾

لِيَجْعَلَ مَا يُلْقِي الشَّيْطَانُ فِتْنَةً لِلَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ وَالْقَاسِيَةِ قُلُوبُهُمْ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَفِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ ﴿٦٤﴾

وَلِيُعَلِّمَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَيُؤْمِنُوا بِهِ فَتُخْبِتَ لَهُ قُلُوبُهُمْ وَإِنَّ لِلَّهِ لَهُدَى الَّذِينَ آمَنُوا إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٦٥﴾

52. Muradi wa maneno haya ni kuwa kila Mtume — na kila mwema — akileta ya kheri, Shetani hujitahidi kutia wasiwasi katika nyoyo za watu kuwa hayo siyo ndiyo, na kuwa ya ndiyo ni hayo waliyo nayo. Hujitahidi mashetani — wa Kibinaadamu na wa Kijini — kutia haya katika nyoyo za wengi. Lakini mwisho wake Mwenyezi Mungu anawaondosha kiwingu hicho, ikawatanzukia haki, wakaifuata. Basi wema wasivunjike nyoyo yanapopingwa wanayoyasema. Inakuja siku ya kuonekana kweli, idumu siku hiyo chungu ya myaka. Basi Mla ni mla leo — na kesho na baadaye. Mla jana amekula nini? Pasemwe:—

Mliyonena uwongo  
Yamekwisha vunja ungo  
Hayatapewa mgongo

Sasa kweli yamekuwa  
Kote yanapiganiwa  
Ila yatang'ang'aniwa.

55. Na wataendelea wale waliokufuru kuwa katika wasiwasi kwa hilo (ulilokuja nalo) mpaka Kiama kiwajie kwa ghafla, au iwajie adhabu ya siku isiyokuwa na kheri (nao hata kidogo).

56. Ufalme siku hiyo utakuwa wa Mwenyezi Mungu (tu peke yake). Atahukumu baina yao. Basi wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri watakuwa katika mabustani (Pepo) yenye neema.

57. Na waliokufuru na kuzikadhibisha Aya zetu, basi hao watapata adhabu ifedheshayo.

58. Na wale waliohama kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu, kisha wakauawa au wakafa (bila ya kuuawa), bila shaka Mwenyezi Mungu atawaruzuku (Kiama) riziki njema (kabisa), na hakika Mwenyezi Mungu ni Mbora wa wanaoruzuku wote.

59. Atawaingiza mahali watakapoparidhia. Na bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mpole.

60. Ndiyo namna hivi. Na ajilipizaye kisasi sawa na dhara aliyotiwa, kisha akadhulumiwa tena, bila shaka Mwenyezi Mungu atamsaidia. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha (na) Mwingi wa maghufira.

61. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu huingiza usiku katika mchana, na Huingiza mchana katika usiku, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona.

62. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu yuko; na wale wanaowaabudu badala yake (Mwenyezi Mungu) hao ni batili, na Mwenyezi Mungu ndiye aliye juu na ndiye Mkubwa.

63. Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu huteremsha maji kutoka mawinguni, na mara ardhi inakuwa chanikiwiti? Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua yaliyofichikana na Mwenye kujua yaliyo dhahiri.

64. Ni Vyake (peke yake vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi na Mwenye kusifiwa.

65. Je! Hukuona kwamba Mwenyezi Mungu amevitiisha kwa ajili yenu vilivyomo ardhini, na (amekutiishieni) marikebu zinazopita baharini kwa amri yake, na amezishikilia mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa idhini yake. Kwa yakini Mwenyezi Mungu kwa watu ni Mpole Mwenye rehema.

وَلَا يَزَالُ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي مَرْيَةٍ مِّنْهُ  
حَتَّىٰ تَأْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً أَوْ يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ  
يَوْمٍ عَقِيمٍ ﴿٥٥﴾

الْمَلِكُ يَوْمَئِذٍ لِلَّهِ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ فَالَّذِينَ  
آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿٥٦﴾

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا فَأُولَٰئِكَ لَهُمْ  
عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿٥٧﴾

وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ قُنُوتُوا  
أَوْ مَاتُوا لَبِّرُوا لَهُمْ اللَّهُ رِزْقًا حَسَنًا وَإِنَّ  
اللَّهَ لَهُ خَيْرُ الرَّزُقِينَ ﴿٥٨﴾

لِيَدْخُلَنَّهُمْ مِّنْ دَحَلٍ مُّبْرُؤُونَ لَهُ وَإِنَّ اللَّهَ  
لَعَلِيمٌ حَلِيمٌ ﴿٥٩﴾

ذَٰلِكَ : وَمَنْ عَاقَبَ بِبِئْسَ مَا عَوَّبَ بِهِ  
ثُمَّ بَعَثْنَا عَلَيْهِ لِيَبْصُرَهُ إِنَّ اللَّهَ لَعَفُورٌ  
غَفُورٌ ﴿٦٠﴾

ذَٰلِكَ يَا أَيُّهَا اللَّهُ يُورِثُ الْيَتِيمَ فِي النَّهَارِ وَيُورِثُ  
النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ وَإِنَّ اللَّهَ لَسَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٦١﴾

ذَٰلِكَ يَا أَيُّهَا اللَّهُ هُوَ الْحَقُّ وَإِنَّ مَا يَدْعُونَ مِنْ  
دُونِهِ هُوَ الْبَاطِلُ وَإِنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ ﴿٦٢﴾

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً  
فَنُصِبَ بِهِ الْأَرْضُ فَخَضِرَتْ إِنَّ اللَّهَ لَطَبِيفٌ حَسِيمٌ ﴿٦٣﴾

لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَإِنَّ اللَّهَ  
لَهُوَ الْعَلِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٦٤﴾

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ  
وَأَلْفَلَاكَ تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ وَيُسَبِّحُ  
السَّمَاءَ أَنْ تَقَعَّ عَلَى الْأَرْضِ إِلَّا بَإِذْنِهِ  
إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرُؤُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٦٥﴾

66. Naye ndiye aliyekuhisheni kisha atakufisheni, kisha atakufufueni. Hakika mwanadamu ni mwizi wa fadhila.

67. Kila uma tumeujaalia kawaida ya ibada wanayoishika. Basi wasishindane nawe katika jambo hili. Na walinganie watu kwendea (dini ya) Mola wako. Bila shaka wewe uko juu ya uwongozi ulio sawa kabisa.

68. Na kama wakiendelea tu kujadiliana nawe, (wakibishana nawe), basi sema: "Mwenyezi Mungu anajua yote mnayoyatenda."

69. "Mwenyezi Mungu atahukumu baina yenu siku ya Kiama katika yale mliyokuwa mkikhitalifiana."

70. Je! Hujui ya kwamba Mwenyezi Mungu anajua yaliyoko mbinguni na ardhini? Bila shaka (yote) hayo yamo Kitabuni (mwake); Hakika (kudhubutu) hayo kwa Mwenyezi Mungu ni sahali.

71. Na wanawaabudu badala ya Mwenyezi Mungu (miungu) ambayo (Mwenyezi Mungu) hakuiteremshia amri (ya kuabudiwa), na ambayo hawana ujuzi nao; Na madhalimu hawatakuwa na wa kuwasaidia.

72. Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi, utaona chuki juu ya nyuso za wale waliokufuru. Hukaribia kuwashambulia wale wanaowasomea hizo Aya zetu. Sema: "Je! Nikuambieni yaliyo mabaya zaidi kuliko haya? Ni Moto Mwenyezi Mungu aliowaahidia wale waliokufuru, na ni marejeo mabaya hayo."

73. Enyi watu! unapigwa mfano, basi usikilizeni; hakika wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu hawawezi kuumba (hata) nzi, wajapokusanyika kwa jambo hili. Na kama nzi akiwanyang'anya kitu hawawezi kukipokonya kwake. Amedhoofika kweli kweli huyu mtaka (kupokonya) na mtakwa (kupokonywa), atakaye na anayetakiwa.

72. Wako katika khatari kubwa kabisa Waislamu wanapoambiwa "Mungu amesema hivi" au "Miume amesema hivi," "Basi wacheni hayo mliyonayo mliyowakuta nayo wazee wenu au Masharifu wenu au Mashekhe wenu au Makhalifa au . . ." Wanapoambiwa haya wakakasirika na kuwashambulia hivi. Basi watu hao wamo katika khatari kubwa kabisa. Na wako watu namna hawa. Basi nawatahadhari kweli kweli au yatawafika yaliyotajwa katika hii Aya ya 72, yatakayowafika makafiri — ingawa wao si makafiri. Lakini hivi ndivyo ilivyo; kuwa: "Kullu Ayatin waradat alal kuffari Tajuru Bidhaylihaa alaa Usatil Muuminin" yaani kila Aya iliyowateremkia makafiri inawakamata na Waislamu wanaofanya kama hayo.

73. Haya jamaa wanaoyaomba makaburi na mzimu na . . . ! Haya siyo yaliyo nayo hayo makaburi na mizimu na . . . ?

وَ هُوَ الَّذِي أَحْيَاكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ۗ إِنَّ الْإِنْسَانَ لَكَفُورٌ ﴿٦٦﴾

لِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنْسَكًا هُمْ نَاسِكُوهُ فَلَا يُنَازِعُونَكَ فِي الْأَمْرِ وَإِذْعَارِي رَبِّكَ إِنَّكَ لَعَلَّ هَذِهِ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦٧﴾

وَإِنْ جَدَلْتَهُمْ فَقُلْ اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٦٨﴾

اللَّهُ يَخْتَصِمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٦٩﴾

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ إِنَّ ذَلِكَ فِي كِتَابٍ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧٠﴾

وَيَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَمْ يَنْزِلْ بِهِ سُلْطَانًا وَمَا لَيْسَ لَهُمْ بِهِ عِلْمٌ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ نَصِيرٍ ﴿٧١﴾

وَإِذَا تُنْتَلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ نَعْرِفُ فِي وُجُوهِ الَّذِينَ كَفَرُوا الْمُنْكَرَ يَكَادُونَ يَسْطُونَ بِالَّذِينَ يَثْلَوْنَ عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا قُلْ أَفَأَنْتُمْ بِشِرْكِنَا مِنْ دُونِ النَّارِ وَعَدَّاهَا اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا وَبَشِّرِ الْمَصِيرِينَ ﴿٧٢﴾

يَأْتِيهَا النَّاسُ ضُرْبَ مَثَلٍ فَاستَمْعُوا لَهُ ۗ إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَنْ يَخْلُقُوا ذَبَابًا وَلَوْ اجْتَمَعُوا لَهُ ۗ وَإِنْ يَسْلُبْهُمُ الذُّبَابُ شَيْئًا لَا يَسْتَنْقِذُوهُ مِنْهُ ضَعُفَ الطَّالِبِ وَالْمَطْلُوبِ ﴿٧٣﴾

74. Hawamuadhimishi Mwenyezi Mungu kama anavyostahiki kuadhimishwa. Hakika Mwenyezi Mungu bila shaka ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda.

75. Mwenyezi Mungu huchagua Mitume miongoni mwa Malaika na miongoni mwa binadamu. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona.

76. Anayajua yaliyo mbele yao (viumbe) na yaliyo nyuma yao, (yaliyopita na yanayokuja). Na kwa Mwenyezi Mungu yatarudi mambo yote.

77. Enyi mlioamini! (Salini) rukuuni na sujuduni na mwabuduni Mola wenu na fanyeni mema, ili mpate kufaulu (kufuzu).

78. Na ipiganieni dini ya Mwenyezi Mungu kama inavyostahiki (kupiganiwa). Yeye amekuchagueni (muwe uma ulio bora). Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika dini. (Nayo dini hii) ni mila ya baba yenu Ibrahimu; Yeye (Mwenyezi Mungu) alikwiteni Waislamu tangu (katika vitabu vya zamani) huko; na katika (Qurani) hii pia (mumeitwa jina hilo), ili awe Mtume shahidi juu yenu na nyinyi muwe mashahidi juu ya watu (wote). Basi simamisheni Sala na toeni Zaka na shikamaneni pamoja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mola wenu. Mola Mwema aliyoje, na Msaidizi Mwema aliyoje!

مَا قَدَرُوا اللَّهَ حَتَّى قَدَرَهُ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٥٥﴾

اللَّهُ يَصْطَفِي مِنَ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا وَمِمَّنَ النَّاسِ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٥٦﴾

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٥٧﴾


يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا ارْكَعُوا وَاسْجُدُوا وَعَبُدُوا رَبَّكُمْ وَارْكَعُوا الْخَيْرَ لَكُمْ تَفْلِحُونَ ﴿٥٨﴾

وَجَاهِدُوا فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ هُوَ اجْتَبَاكُمْ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ مِلَّةَ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ هُوَ سَمَّاكُمُ الْمُسْلِمِينَ مِن قَبْلُ وَفِي هَذَا لِيَكُونَ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى

النَّاسِ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَاعْتَصِمُوا بِاللَّهِ هُوَ مَوْلَاكُمْ فَنِعْمَ الْمَوْلَى وَنِعْمَ النَّصِيرُ ﴿٥٩﴾

الْحَدِيثُ فِي سُنَنِ ابْنِ أَبِي شَيْبَةَ طَابَتْ لَهُ النَّاسُ

بِجَاءِ



Ina Aya 118

SURATUL MUUMINUN

Inu Makuru 6

(Imeteremka Makka)

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuncemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuncemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

1. Hakika wamefuzu Waislamu
2. Ambao katika Sala zao huwa ni wanyenyekevu
3. Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi
4. Na ambao (nguzo ya) Zaka wanaitekeleza
5. Na ambao tupu zao wanazilinda
6. Isipokuwa kwa wake zao au kwa (wanawake) wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, (kulia). Basi hao ndio wasiolaumiwa.
7. (Lakini) anayetaka kinyume cha haya, basi hao ndio warukao mipaka (ya Mwenyezi Mungu).
8. Na ambao amana zao na ahadi zao wanaziangalia, (wanazitekeleza)
9. Na ambao Sala zao wanazihifadhi.
10. Hao ndio warithi
11. Ambao watarithi Pepo; wakae humo milele.
12. Na kwa yakini tulimuumba mwanadamu kwa udongo ulio safi.
13. Kisha tukamuumba kwa tone la manii, (mbegu ya uzazi) lililowekwa katika makao yaliyohifadhika.
14. Kisha tukalifanya tone hilo kuwa pande la damu, na tukalifanya pande la damu hilo kuwa pande la nyama, kisha tukalifanya pande la nyama hilo kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama, kisha tukamfanya kiumbe kingine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.
15. Kisha hakika nyinyi baada ya hayo ni wenye kufa.

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ①  
 الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ ②  
 وَالَّذِينَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ③  
 وَالَّذِينَ هُمْ لِلزَّكَاةِ فَاعِلُونَ ④  
 وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ ⑤  
 إِلَّا عَلَىٰ أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ ۚ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْعَدُونَ ⑥  
 وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمْتِنِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ⑦  
 وَالَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَوَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ ⑧  
 أُولَٰئِكَ هُمُ الْوَارِثُونَ ⑨  
 الَّذِينَ يَرِثُونَ الْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ⑩  
 وَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ مِنْ سُلَالَةٍ مِّن طِينٍ ⑪  
 ثُمَّ جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ مَّكِينٍ ⑫  
 ثُمَّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَاقَةً ۖ فَخَلَقْنَا الْعَاقَةَ مَضْغَةً ۖ فَخَلَقْنَا الْمُضْغَةَ عِظْمًا ۖ فَكَوْنَا الْعِظْمَ رِجْسًا ۚ  
 ثُمَّ أَنشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ ۖ فَتَبَرَّكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ ⑬  
 ثُمَّ إِنَّمَا بَعَدَ ذَلِكَ لَيْسُونَ ⑭

15, 16. Katika maelezo ya Aya hizi walizozifanya kuwa ni ya 16 na 17 wamepachikia tena kuwa aliyekufa hawezi kurejea, ili wapinge yale maneno ya Mtume yaliyosihhi kuwa Nabii Isa atarejea ulimwenguni. Sisi hatuwezi kumkhalifu Mtume kwa maneno ya watu wengine.